Shule za Umma za Aurora
Eneo la Kuchukua HATUA la MMM
Agosti 21, 2015

**Eneo la Kuchukua HATUA ni nini?**
Katika kwenda sambamba na mpangokazi wa APS, APS 2020: Kufinyanga Siku za Usoni na Mpango Sanifu wa Eneo la kuchukua HATUA, APS inapendekeza kuimarisha Eneo moja la kuchukua HATUA mwaka huu, na hadi maeneo matatu ya kuchukua HATUA katika miaka ijayo. Kila Eneo la kuchukua HATUA litakuwa na kiungo chenye mada miongoni mwa shule, na shule zote ndani ya eneo moja zitaweza kugawiza baadhi ya sifa hizo kuu. Kila shule katika eneo husika itakuwa na fursa ya kuendeleza mpango wake binafsi-mahsusi. Mipango hii itakuwa sehemu ya utumaji ombi wa kupata Hali ya Shule katika Ugunduzi Colorado. Maombi haya na kila usanifu mpya wa shule yatahitajika kuonyesha waziwazi na kwa usahihi namna ambavyo shule itakavyotumia uhuru wake katika kutumia wafanyakazi, muda, pesa, na programu ambazo zinaandamana na shule kupata hali hiyo ya ugunduzi ili kuweza kuendesha manufaa kwa mafanikio ya mwanafunzi.

**Akronimu *MJAMUF* katika Maeneo ya kuchukua HATUA inamaanisha nini?**
Akronimu ya *MJAMUF* katika Maeneo ya kuchukua HATUA inamaanisha **M**tandao utokanao na **J**amii ya **A**urora unaoleta **M**ageuzi, **U**gunduzi na **F**ursa.

**Je uundaji wa Eneo la kuchukua HATUA uliamrishwa na Jimbo?**
Eneo la kuchukua HATUA **haliku**amrishwa na Jimbo. Wilaya nyingi kotekote nchini zimeweza kutekeleza miundo kama hii kama njia ya kuonyesha ugunduzi na usanifu mpya wa shule katika kushirikiana na jumuia; kuondoa vizuizi halisi au fikiriwa; na kuboresha kisawasawa na kwa haraka fursa za kusoma na mafanikio ya wanafunzi.

**Ni kwa nini shule zinatafuta kuwa katika hali hiyo ya Ugunduzi kama sehemu mojawapo ya Eneo la kuchukua HATUA?**
Shule na wilaya zimekumbana na changamoto katika kuzidisha mafanikio ya mwanafunzi. Hali ya ugunduzi itawezesha shule zilizo katika Eneo la kuchukua HATUA kuweza kufikiria tofauti na kusanifu upya miundo ya shule zao ili kuzidisha mafanikio kwa wanafunzi wote, ili wanafunzi wetu waweze kufinyanga siku za usoni zenye ufanisi.

**Kuwa katika Hali ya Ugunduzi kunamaanisha nini?**
Kuwa katika hali ya ugunduzi katika jimbo kunaruhusu shule kubakia kwenye wilaya huku ikizidi kupatia jumuia unyumbukaji wa ziada ili kuweza kujisanifu. Hali ya ugunduzi inaruhusu shule kuweza kuunda mpango maalum na wa kipekee wa miundo, programu na mifumo ya utawala ambayo itaweza kuwahudumia wanafunzi kwa njia bora zaidi shuleni. Unahitaji jumuia nzima ya shule kushirikiana katika kutekeleza mipango ya ugunduzi ili kuimarisha mafanikio ya mwanafunzi ambayo yanaweza kuathiri watu, muda, programu au pesa. Baada ya hayo kufanyika, shule nayo itaweza kutojumuishwa katika sheria fulani za jimbo au sera fulani za shule ya wilaya ili kuweza kutekeleza mpango wa ugunduzi. Shule za ugunduzi zilizoidhinishwa na jimbo zinawezeshwa na Kifungu cha Sheria cha Ugunduzi shuleni 2008.

**Maeneo ya kuchukua HATUA yako vipi tofauti na shule nyingine za ugunduzi katika APS kama vile Shule Anzilishi, Shule za Kusoma masomo ya Ziada na Shule za Mkataba?**
Maeneo ya kuchukua HATUA yanaendeleza msingi wetu wa sasa wa kuunda shule za mkataba, anzilishi na za ugunduzi-wilayani. Mfumo wa eneo la kuchukua HATUA unaweka pamoja mahitaji, mashabaha na mazingatio ya jumuia ya shule katika eneo pamoja na mashabaha na imani kuu ya mpangokazi wa shule ya wilaya, APS 2020: Kufinyanga Siku za Usoni. Eneo la kuchukua HATUA litasanifiwa ili kuweza kushughulikia mahitaji mahsusi ya jumuia kwa kutumia ugunduzi na rasilimali lengwa. Linatoa msingi wa kunyumbuka na maalum ambao unaangazia uwezo wa kipekee na hali za wanafunzi katika shule zinazopatikana kwenye eneo husika.

**Shule zinashiriki vipi katika Eneo la kuchukua HATUA?**

- Eneo la kuchukua HATUA la kwanza katika Shule za Umma za Aurora litajumuisha shule zinazotimiza mipangilio miwili mikuu:
    - Lazima shule hizi ziwe katika mpangilio wa ulishaji wa Shule ya Upili Kuu ya Aurora.
    - Lazima shule zilingane na mada ya Eneo la kuchukua HATUA.

- Mpaka pale mada yatachaguliwa na Kamati ya Ushauri wa Eneo, shule zote katika mpangilio wa ulishaji wa Shule ya Upili Kuu ya Aurora zitapokea taarifa kuhusu fursa hii ya kushiriki katika Eneo la kuchukua HATUA.

**Washikadau wakuu ni kina nani au watakaohusika katika mchakato ni kina nani?**

- Elimu ya Mass Insight
- Kamati ya Ushauri ya Eneo
- Timu ya Usanifu wa Eneo
- Timu ya Usanifu wa Shule

**Elimu ya Mass Insight ni nini?**
Elimu ya Mass Insight ni marekebisho ya elimu ya shirika lisilo la faida ambalo linafanya kazi na shule binafsi, shule za wilaya na linaweka wazi suala la kusanifu upya shule zao zinazofanya vibaya zaidi na kupatia nguvu wilaya ili kuweza kuwahudumia wanafunzi wanaohitaji msaada.

**Mass Insight kwa umma ndio itakayoendesha shule zetu?**
Mass Insight si shirika la mkataba na haliendeshi shule kivyake. Mass Insight ni shirika linaloamini kwamba kunao wajibu thabiti kwa wilaya kuweza kuchukua na kulenga kusaidia wilaya katika namna ambavyo inavyosaidia wanafunzi na familia.

**Kamati Shauri ya Eneo ni nini?**

- Kamati Shauri ya Eneo (ZAC), ambayo inateuliwa naye Msimamizi wa shule wa APS ni kundi la viongozi wa eneo, wenye asili mbalimbali na walio na muunganisho thabiti katika

Aurora Asilia na walio na maarifa kuhusu fursa za kiuchumi na baada ya sekondari zinazopatikana kwa wale wanaohitimu APS. Wajibu wa kwanza wa ZAC ni kuweza kutathmini na kuchagua mada ya Eneo la kuchukua HATUA.

- Pindi mada yatakapochaguliwa, Kamati Shauri ya Eneo itakuwa na wajibu mara mbili:
    - Kutoa pendekezo kwake Msimamizi wa shule kuhusu kama ombi la eneo husika linatimiza au halitimizi mpangilio uliowekwa mbele yake kwa kadri ambavyo ombi linavyoenda mbele kutoka kwenye timu ya usanifu wa shule hadi kwenye Kamati ya Elimu ya APS
    - Saidia Msimamizi wa shule katika kuwasilisha maombi ya ugunduzi katika Kamati ya Elimu ya Jimbo la Colorado

**Ni nani aliye katika Kamati ya Ushauri wa Eneo?** Wanachama wa Kamati ya Ushauri wa Eneo wanajumuisha Norm Brownstien, Jim Kelley, Mariana Ledezma-Amorosi, Mary Lewis, Ruben Medina, George “Skip” Noe, Dkt. Betsy Oudenhoven, Maisha Pollard, Karen Porter na Aaron Thompson**.**

- Tazama tawasifu za wanachama wa Kamati ya Ushauri wa Eneo.

**Timu ya Usanifu wa Eneo ni nini?**

- Timu ya Usanifu wa Eneo, ambayo inateuliwa naye Msimamizi wa shule na viongozi wa shule, inajumuisha washikadau walioteuliwa kutoka katika kategoria tatu:
    - Wafanyakazi wa shule
    - Wafanyakazi wa wilaya
    - Washikadau wakuu
- Timu ya Usanifu wa Eneo itaweza:
    - Kuunda mchakato wa kutuma maombi ya ugunduzi na kazi ya usanifu ya shule
    - Kupatia shule msaada wakati wa mchakato huu
    - Kuhakikisha kwamba usanifu wa shule na maombi ya ugunduzi yanafikia ubora unaotosha ili kupendekeza Kamati ya Elimu ya APS na Kamati ya Elimu ya Jimbo la Colorado

**Timu ya Usanifu wa Shule ni nini?**

- Timu za Usanifu wa Shule zitaweza kuitwa pamoja baada ya shule kuonyesha nia ya kujiunga katika eneo husika na kujaza utathmini wa shule kuwa tayari ambayo ni uhakiki wa mfumo wa shule ili kusaidia mfanyakazi na wanafunzi na ubora wa maelekezi.

- Timu za Usanifu wa Shule zitawakilisha jumuia ya shule kwa ujumla na zitajumuisha:
    - Wafanyakazi wa shule
    - Wazazi
    - Wanafunzi (pale panapofaa)
    - Washikadau wakuu

- Timu za Usanifu wa Shule zitaweza:
    - Kuchambua Utathmini wa Shule kuwa Tayari na nyaraka nyingine zinazofaa
    - Kuamua machaguo ya usanifu wa shule ambayo yanalingana na mpangilio wa Eneo la kuchukua Hatua
    - Kuandika maombi ya hali ya ugunduzi wa jimbo
    - Kujaza usanifu wa shule na kuiwasilisha katika Timu ya Usanifu wa Eneo

**Utathmini wa Shule kuwa Tayari ni nini?**
Tathmini za shule kuwa tayari, zinazofanywa na Mass Insight, ni uhakiki wa uwezo wa shule kuweza kusaidia mfanyakazi na wanafunzi na kuongoza pamoja na kusimamia mabadiliko. Tathmini za kuwa tayari zitatumika na vinara wa shule na wakurugenzi wa P-20 ili kusaidia shule kuweza kupangilia timu zao za usanifu.

**Kipimo cha muda cha usanifu upya wa shule ni kipi?**
Tathmini za shule kuwa tayari zitaweza kufanyika mwishomwisho wa mwezi wa Agosti na mwanzomwanzo wa mwezi wa Septemba. Jumuia za shule ambazo zingependa kuchunguza uwezekano wa ugunduzi zitaweza kuanza mchakato wa kusanifu upya mwishomwisho wa mwezi wa Septemba na kuendelea hadi msimu wa mapukutiko. Shabaha ni kuwa na usanifu mpya wa shule na kurasimu maombi ya ugunduzi yaliyotayarishwa na kusaidiwa na jumuia za shule mnamo Januari 2016. Kimsingi, Kamati ya Elimu ya Shule za Umma za Aurora itakuwa na fursa ya kuhakiki usanifu mpya na maombi kwenye msimu wa kipupwe wa mnamo 2016, na kuwasilisha nyenzo husika katika Kamati ya Elimu ya Jimbo la Colorado hapo baadaye.

**Je mabadiliko yatakuwepo mara moja katika mfumo wa shule yetu?**
Kila mwaka, shule zitafanya uboreshaji katika njia ambayo itawawezesha kuwaunga mkono wanafunzi wao na familia. Hata hivyo, usanifu mpya ambao huenda ukapendekezwa katika utumaji ombi la ugunduzi hautakuwa umeonwa hapo kwa hapo, na shabaha ni kuweza kuanza mwaka wa shule wa 2016-17 kwa mifumo mipya ya shule.

**Nani ndiye hutoa uamuzi wa mwisho katika Hali ya Ugunduzi wa Jimbo?**
Lazima hali ya ugunduzi wa shule iidhinishwe na Kamati ya Elimu ya APS na Kamati ya Elimu ya Jimbo.

**Wazazi wanawezaje kushiriki?**
APS inathamini mchango wa wazazi na msaada kwa kila mwanafunzi anayesoma. Wazazi huwa na wajibu mkuu katika usanifu mpya wa shule na namna ambavyo APS inavyosaidia Eneo la kuchukua HATUA kwa ujumla. Uwakilishi wa mzazi utakuwepo katika Kamati ya Ushauri wa Eneo, na wazazi wataweza kuhudumu pia katika Timu za Usanifu wa Shule. Maoni kutoka kwa wazazi siku zote yanakaribishwa na ni muhimu kwa kadri shule zinavyofikiria upya namna zitakavyohudumia wanafunzi wake. Shule za APS na wafanyakazi wa wilaya watatafuta mchango wa mzazi kotekote kwenye mchakato huu. Mikutano ya jumuia itaweza kuratibiwa ili kuwapatia wazazi habari za mara kwa mara na kuwapa fursa ya kutoa michango na kuwauliza maswali viongozi wa shule na wilaya.

**Wajibu wa walimu na wafanyakazi wa shule katika Eneo la kuchukua HATUA katika shule ni upi katika kuidhinisha usanifu mpya wa shule?**
Kwa mujibu wa sheria ya Colorado, walimu na wafanyakazi wa shule lazima walikubali ombi la ugunduzi. Kama ombi la ugunduzi litapendekeza mabadiliko katika kazi zao, matoleo hayo ya ombi lazima yaweze kupigiwa kura.

**Kipimo cha muda cha uidhinishwaji wa ugunduzi ni kipi?**
Inawezekana kwamba maombi ya ugunduzi yataweza kuwasilishwa katika kamati za APS na ile ya elimu ya Jimbo kwenye msimu wa kipupwe au machipuko mnamo 2016. Kamati zitahakiki maombi na kuidhinisha au kukataa hali ya Eneo la kuchukua HATUA katika shule hapo baadaye.